**NAMBA 2: MARKO 4:1–20: MFANO WA MPANZI. KUPANDA MBEGU YA INJILI**

Kama tunapoanza kipindi kingine, hebu turejee kwenye kitabu cha **Marko sura ya nne**, na tutasoma mstari wa kwanza hadi ishirini. Mfano wa Mpanzi. Hii ni habari ambayo tunaijua vyema. Na pia ni mfano ambao tunauelewa vizuri, kwa sababu watu wengi nchini Tanzania wanajua kuhusu mambo ya kilimo. Watu wengi wanalima vyakula vyao wenyewe. Watu wengi wana viwanja vya ardhi ambavyo wanavilima ili kujipatia chakula. Watanzania wengi hupanda mbegu zao wenyewe. Wao huyatunza mazao yao kwa kuyamwagilia, na katika wakati wa kuvuna, wao huyakusanya mazao, na kwa namna hiyo wanajipatia chakula kwa ajili yao na familia zao. Watanzania, kama ilivyo kwa watu wengi katika Agano Jipya, wanajua jinsi ya kupanda mbegu. Lakini kama utaenda Uingereza au Marekani, watu wengi hawajui kuhusu kilimo. Hawana mashamba yao wenyewe. Wao hawapandi vyakula vyao wenyewe. Kwa kweli wao hudhani chakula chao hutoka kwenye maduka makubwa, na siyo shambani! Lakini nina uhakika kuwa ninyi nyote mnajua vizuri kuhusu mambo ya kilimo.

Kifungu ambacho sisi tunakiangalia sasa, ni juu ya mkulima ambaye alipanda mbegu. Nanyi kama wachungaji na wainjilisti, Mungu anakutarajia uwe mkulima. Anakutarajia wewe upande mbegu. Ni aina gani ya mbegu? Anakutarajia wewe upande mbegu za injili katika akili za watu wako. Anakutarajia wewe uwe mkulima wa Mungu! Wakati mwingine, katika huduma yako, unaweza ukajikuta kwamba unapopanda mbegu katika kanisa lako, hakuna matunda – na jambo hili linaweza kukatisha tamaa. Lakini wakati mwingine, pale unapofundisha injili kwa watu, kuna kukawa na matunda mengi, na jambo hili kutia moyo - kama vile inavyotia moyo kwa mkulima pale, anapoona mimea yake, ikikua vizuri shambani. Natumaini kwamba, tunapojifunza leo, utajifunza kitu kipya kuhusu aina nne tofauti za udongo, ambazo Yesu anazizungumzia. Hivyo hebu tusome **Marko sura ya nne, mstari wa kwanza hadi ishirini.**

Katika sehemu hii ya injili, Yesu ni mwalimu maarufu. Alikuwa ameanza tu huduma yake, lakini tayari watu walikuwa wakisafiri kilometa nyingi, ili waweze kumwona. Hadi sasa, Yesu katika huduma yake, alikuwa amefanya mambo **matatu** tofauti. Amewaponya wagonjwa. Amewafungua watu kutoka kwenye mapepo, na amefanya mengi ya mafundisho juu ya ufalme wa Mungu. Katika **sura ya kwanza** Yesu anakemea mapepo yamtoke mtu katika sinagogi huko Kapernaumu. Pia katika **sura ya kwanza** tunaambiwa kwamba, Yesu aliwaponya watu wengi huko Kapernaumu, ikiwa ni pamoja na mama mkwe wake na Petro, na mtu mwenye ukoma.
Katika **sura ya pili** tunajifunza kwamba kulikuwa na mtu aliyeshushwa chini kupitia katika paa la nyumba, na alipona na Yesu. Katika **sura ya tatu** Yesu anamponya mtu mwenye mkono uliopooza. Mtu huyo hakuweza kuutumia mkono wake – ulikuwa umekufa; hakuweza hata kuusogeza – lakini Yesu akamponya. Kwa sasa aliweza kuutumia mkono wake tena.

Na kwa kweli, wakati watu walipoiona miujiza hii, walishangazwa. Kama utauona muujiza utashangaa, na unaweza kuwaambia marafiki zako juu ya muujiza huo. Unaweza kuwapigia simu na kuwaambia. Ni kitu kile kile tunakiona hapa katika injili ya Marko, wakati watu walipo-iona miujiza ya Yesu, waliwaambia watu wengine, na hivyo watu zaidi na zaidi walikuja kumtafuta Yesu, kwa sababu walitaka kuona miujiza zaidi na zaidi. Na hapa katika **mstari wa kwanza**, umati ambao ulikuwa umekusanyika kando ya ziwa, ulikuwa mkubwa sana, mpaka ilimlazimu Yesu kuingia katika mashua, ili aweze kuwafundisha watu.

Je, unaweza kufikiria jinsi ilivyo ukihubiri ukiwa kwenye mashua?! **Mstari wa pili** unatuambia kwamba Yesu alifundisha vitu vingi kwa kutumia mifano. Lakini kabla ya kuiangalia mifano

gani, hebu niseme kitu muhimu kuhusu mafundisho ya Yesu. Katika huduma yake, Yesu aliwaponya wagonjwa na kutoa pepo wabaya kutoka kwa watu. Mambo haya mawili yaliwasaidia watu kwa njia ya kimwili. Kwa nyakati chache pia alifanya miujiza kutoa chakula kwa watu waliokuwa na njaa ili wapate kula. Miujiza hii yote iliwasaidia watu kimwili, na inaonyesha kwamba Yesu alikuwa na huruma kwa watu kwa mahitaji yao ya kimwili. Aliwajali na alitaka kuwaponya. Na hii ndio sababu umati wa watu ulikuwa unamfuata. Walitaka kuponywa magonjwa yao.

Lakini vitu hivi havikuwa vitu muhimu sana katika huduma ya Yesu. Je, unadhani ni kitu gani kilichokuwa ni cha muhimu zaidi? Kuhubiri na kufundisha kuhusu ufalme wa Mungu. Unaweza kuona, watu wote ambao walikuwa wameponywa na Yesu, hatimaye walikufa. Walikuwa wameponywa na maisha yao yaliboreshwa kwa miaka michache; labda waliishi kwa miaka kumi, ishirini au thelathini zaidi, lakini hatimaye waliweza kufa, kwa sababu ya uzee wa umri au ugonjwa. Uponyaji wao wa kimwili ulikuwa ni wa muda tu. Lakini Neno la Mungu lenyewe linaishi milele; ufalme wa Mungu huishi milele; nafsi zetu huishi milele kwa sababu sisi ni viumbe vya kiroho pia. Kwa hiyo, ni kipi kilicho cha muhimu zaidi? Kimwili au kiroho? Hivyo basi tunahitaji kitu ambacho kitakusaidia sisi kuhusiana na roho zetu. Tunahitaji kitu ambacho kinatufundisha kuhusu ufalme wa Mungu. Tunahitaji kuisikia injili. Watu wanahitaji kusikia kuhusu msalaba na ufufuo. Je, wao wanasikia hii habari njema – kupitia mahubiri na mafundisho. Ujumbe wa injili ni ujumbe muhimu zaidi ulimwenguni. Unatusaidia kuelewa ni kwa nini Yesu alikuja. Unatuambia kuhusu msalaba. Unatuambia jinsi tunavyoweza kuokolewa, si kimwili, bali kiroho – na hili ni jambo muhimu zaidi kuliko mambo ya kimwili.

Ninafikiri kuna hatari kwa baadhi ya makanisa, ambayo hutumia muda mwingi kushughulikia ya mambo ya kimwili, lakini hayatumii muda wa kutosha kwenye mambo ya kiroho. Kanisa linaweza kutoa vyakula kwa jamii katika wakati wa uhitaji. Kanisa linaweza kuwa na mpango wa kuelimisha watoto. Watu wa Kanisani wanaweza kuwatembelea wagonjwa. Mambo hayo yote ni mazuri. Ni mambo ambayo Kanisa lazima liyafanye, lakini kama Kanisa linawasaidia watu kimwili tu, watakuwa wameliacha lengo kuu. Watu hawa watakuwa wameliacha kusudi muhimu zaidi! Na kusudi hilo ni kuwasaidia watu kiroho. Sisi kama wachungaji na wainjilisti, tunatumiaje muda mzuri kuwafundisha watu wetu, au je, tunashughulikia sana katika kukidhi mahitaji ya kimwili ya watu wetu? Je, waweza kuona kile ninachojaribu kukisema?

Kanisa linahitaji kuwa na usawa ulio mzuri. Kuna haja ya kuwa na kazi njema, lakini pia kuna haja ya kuwa na mafundisho mazuri. Tunaposoma injili, tunaona kwamba Yesu mara nyingi aliwachukua wanafunzi wake mahali pa utulivu ili kuwafundisha. Alitaka kuwapa mafunzo ya jinsi ya kuwa wanafunzi wema. Mara nyingi Yesu alifundisha katika sinagogi. Alitaka kufundisha habari njema, na hata alifanya hivyo kwa umati wa watu ambao alikuwa pamoja nao. Yesu alisema: *"Nimekuja kuwafundisha juu ya ufalme wa Mungu".*

Na hivyo hapa tunamwona Yesu akiwa kando ya ziwa Galilaya, akifundisha umati jinsi ya kufanya kitu muhimu sana. Kwa njia nyingi, alikuwa mwalimu wa kipekee. Hakuwa na chumba cha darasa kubwa la kufundishia. Hakuwa na kompyuta. Hakuwa na ratiba ya kufundisha. Hakuwa na maktaba ya kujisomea. Hakuwa na ubao wa kufundishia. Na bado alikuwa mwalimu mkuu katika ulimwengu! Moja ya mambo ambayo aliyatumia katika kufundisha, ni kitu kinachoitwa '*mfano*'. Angalia katika **mstari wa pili**: *"Aliwafundisha mambo mengi kwa mifano".* Sasa, vipi kuhusu neno hili '*mfano*'? Linamaanisha nini? Wakati mwingine mifano inaweza kuwa mifupi sana na rahisi sana, lakini daima ni hadithi. Mfano ni hadithi ambayo ni

sehemu ya maisha, na hadithi ambayo pia yana maana yake. Mfano ni hadithi ya kidunia, lakini iliyo na maana ya mbinguni.

Yesu hasemi tu hadithi nzuri – yeye anasimulia hadithi ambayo yana ujumbe wenye nguvu ndani yake. Na wakati Yesu alipokuwa anawambia hadithi, baadhi ya watu walielewa kwamba kulikuwa na ujumbe nyuma ya habari, ambayo waliihusisha katika maisha yao. Aliwataka watu wajiione wenyewe katika mfano. Aliwataka watu wafikirie – Je, hii naweza kuihusisha katika maisha yangu? Na mara nyingi, tunaposoma mifano ya Yesu, ni rahisi kuielewa. Mfano wa kondoo aliyepotea, mfano wa punje ya haradali, mfano wa mwana mpotevu. Hata hivyo, kuna baadhi ya mifano ambayo ni migumu kuielewa. Utaona katika **mstari wa kumi** kwamba wanafunzi hawakuelewa mfano huu hapa katika **Marko sura ya nne**, na hivyo walimwendea ili kumwomba Yesu, na walimsihi awafa-fanulie juu ya mfano huo. Na hivyo kwa bahati nzuri, tunayo maelezo haya mbele yetu leo katika **mistari ya kumi na nne hadi ishirini.**

Kwa nini Yesu aliichagua mfano huu katika tukio hili? Unaona, nafikiri kwamba Yesu alichagua mifano yake kwa makini sana. Anapouangalia umati huu mkubwa mbele yake, anajua kwamba kuna watu walio na viwango tofauti vya imani na uelewa wa kiroho. Watu wengi walikuwa huko walienda kuona muujiza mwingine; kwa kweli hawakupendelea kusikiliza kile ambacho Yesu alikifundisha, bali walitaka kuona muujiza tu. Baadhi ya watu walikuwa pale kwa sababu walikuwa na hamu ya kile ambacho Yesu alikuwa akikisema. Baadhi ya watu walikuwa na njaa ya kulisikia Neno la Mungu, na wengine hawakuwa na njaa kabisa. Baadhi ya watu walikuwa wakimkubali, na waliweka imani zao kwake, lakini wengine katika umati walikuwa wakimkataa. Na hivyo Yesu anawaambia mfano huu kuhusu mkulima, ambaye alitoka nje ili kupanda mbegu – na kuhusu aina **nne** tofauti za udongo ambazo mbegu zilipandwa juu yake.

Tunajua kwamba **mbegu** inayopandwa inawakilisha Neno la Mungu – habari njema ya ufalme. Tunajua kwamba mpanzi ni bila shaka ni Yesu, ingawa inaweza pia kutumika kwa mtu yeyote, ambaye anashiriki katika kufundisha injili, iwe kwa kuhubiri kwa watu wengi katika Kanisa, au kumfundisha mtu mmoja peke yake. Na tunajua kwamba aina tofauti za udongo zinawakilisha hali tofauti za moyo wa mwanadamu, ambazo kwazo mbegu hupandwa. Kwa maneno mengine, mfano huu unahusu njia tofauti za watu wanavyo-uitikia ujumbe wa injili. Kwanza, angalia **Mstari wa kumi na tano**: *"Baadhi ya watu ni kama mbegu iliyo katika njia ambapo, mara tu wakishasilikia Neno, Shetani huja na kuiondoa mbegu, ili wasiweze kukua."* Sasa, mashamba katika Israeli, katika siku hizo, mashamba yalikuwa na ploti ndefu na nyembamba. Katikati ya kila ploti hizo za mashamba, kulikuwa na njia ndogo ndogo ambazo watu waliweza kuzitumia pamoja na wanyama, na mikokoteni yao. Wakati wa msimu wa kiangazi, njia hizi zilikuwa ngumu sana, kwa sababu hapakuwa na mvua.
Zilikuwa ngumu sana, zilikuwa kama zege. Ni sawa hapa Tanzania wakati wa msimu wa kiangazi. Na pale mkulima alipoziweka mbegu kwenye udongo wa nchi, baadhi ya mbegu zinaweza kuanguka kwenye njia ndogo, iliyo kando mwa shamba. Na kwa sababu udongo ulikuwa ni mgumu sana, mbegu hizi haziwezi kukua, kwa hiyo ndege wa angani walikuja na kuzila.

Na Yesu anasema kwamba kuna watu katika ulimwengu, ambao wanafanana kama udongo huu. Wao huizuia injili. Maisha yao ni magumu kama zege la saruji. Hawana hamu yoyote na Ukristo. Kwa kweli, maisha yao ni magumu sana, na hata ukiwaambia kuhusu msalaba na upendo wa Mungu kwao, hauimaanishi chochote. Hawana shauku na Kristo. Hata ukijaribu kuwaelezea injili, bado hawawezi kuiona habari njema - na hata hawataki kuiona! Wakati

mwingine watu hawa ni hata huwa wakali wenye fujo kwa injili. Je, tunapaswa kufanya nini kwa watu hawa? Kama wachungaji na wainjilisti tunafanya nini na watu kama hawa? Labda kuna watu katika familia yako ambao ni kama hawa. Wao ni kama udongo mgumu kwa injili. Labda umekuwa akiwahubiri kwa muda mrefu juu ya Yesu – lakini bado hawajaitikia. Mbegu ya injili imekuwa ikigonga na kukwama kuingia maishani mwao! Wewe endelea kuomba! Endelea kuomba! Endelea kuomba! Mwambie Mungu kuwasaidia.

Ninawajua wamisionari wachache ambao wanaishi na kufanya kazi katika sehemu mbalimbali za ulimwengu, mahali ambapo watu wake hawataki kuikubali injili kwa urahisi. Na wamisionari hawa wamekuwa wakifanya kazi yao kwa miaka mingi – lakini huona matunda madogo sana. Baadhi yao hawajawahi kuona hata mtu yeyote akimjua Yesu. Je, wanaweza kufanya nini? Wao huendelea kuonyesha upendo wa Mungu kwa watu, na wakati wanapopata nafasi, huwa wanaendelea kuhubiri kuhusu upendo wa Mungu. Watu hawa wao huendelea mwaka baada ya mwaka, wakiomba kwamba Mungu aingilie kati katika maisha magumu ya watu hawa. Hayo ndiyo wote tunayoweza kuyafanya. Endelea kuomba tu.

**Pili**, angalia **mstari wa kumi na sita na kumi na saba**. *"Wengine, ni kama mbegu zilizopandwa kwenye maeneo ya miamba, hulisikia Neno, na mara moja hulipokea kwa furaha. Lakini, kwa vile hawana mzizi, hudumu kwa muda mfupi kwani wakati shida unapokuja wao huanguka kwa haraka".* Katika Israeli kuna maeneo mengi ya nchi, ambayo yana udongo usio na kina sana - na kwenda chini kuna sentimita chache tu, kisha kuna safu ya mawe magumu. Wakati mbegu zinapopandwa katika udongo huu, huanza kuweka mizizi yake katika udongo na kukua – lakini kwa sababu udongo hauna kina, mizizi yake hugonga mwamba mgumu, na haiwezi kwenda kwa undani zaidi. Je, matokeo yake ni nini?
Hakuna maji mengi au udongo ili kukuza mmea, na hivyo wakati jua linapoangaza, au upepo mkali unapovuma, mmea huo hukauka na kufa.

Nadhani kwamba sisi tunayaona haya mara nyingi katika makanisa yetu. Watu wanafanya uamuzi wa kumfuata Kristo. Mtu huyo huwa Mkristo. Nao huanza vizuri sana; wakiwa na furaha sana, na wanataka kumwambia kila mtu kile ambacho Yesu amewafanyia. Lakini baada ya miezi michache, au miaka michache, hugeuka na kurudi nyuma, na hatuwaoni tena kanisani. Jambo hili hufanyika wakati wote. Watu wengi huamua kumfuata Kristo – lakini imani yao haina kina sana, na mizizi yao haijaenda chini sana kwenye udongo. Hawaja-mruhusu Yesu kuingia kikamilifu katika maisha yao. Na hivyo, wakati wanapopata shida, huanguka na wakati mwingine huwa na hasira sana juu ya Ukristo. Katika baadhi ya maeneo ya Afrika, injili inaheshimiwa sana, na watu wengi hujiita Wakristo. Pengine hadi asilimia **hamsini** ya watu katika bara la Afrika, hasa kusini mwa **Sahara**, watu hawa husema kuwa ni Wakristo. Lakini, baadhi ya watu hawa, hawajairuhusu mizizi yao iende na kuzama chini na kwa undani katika Kristo.

Acha nikuelezee kile ninachomaanisha hapa. Huko nyuma mnamo mwaka **elfu moja, mia tisa na tisini na nne**, nchi ya **Rwanda** ilikuwa na mauaji ya kimbari. Hiyo ni miaka ishirini na sita iliyopita. Huko Rwanda wakati huo, kulikuwa na makabila mawili – kabila moja liliitwa Watusi, na wengine waliitwa Wahutu. Kulikuwa na kutoelewana kati ya makabila haya mawili, na hivyo baadhi ya Wahutu waliamua kuwaua Watusi wote. Takribani Watusi milioni moja waliuawa. Mhutu angemuua jirani yake wa Mtusi kwa sababu alikuwa ni mtu wa kutoka kabila jingine. Pia jeshi la Wahutu lilijihusisha katika mauaji hayo. Kuna habari nyingi za kile kilichotokea Rwanda wakati huo. Lakini sikiliza hii. Unajua, wakati huo katika nchi ya Rwanda, asilimia **tisini na tatu** ya watu wote wa Rwanda, walidai kuwa walikuwa ni Wakristo! Hiyo ni

idadi kubwa. Ni kwa namna gani mauaji haya yanatokea katika nchi, ambayo karibu watu wote wanadai kuwa ni Wakristo?

Na hii ndiyo hoja yangu. Ikiwa asilimia **tisini na tatu** ya watu walikuwa ni Wakristo halisi, mauaji haya yasingeweza kutokea. Watu wengi walisema kuwa wanamfuata Yesu – lakini imani yao haikuwa na kina sana, na walikuwa hawajamruhusu Yesu katika maisha yao. Ukristo ulikuwa bado haujaathiri mioyo yao. Imani yao ilikuwa haina kina sana kwa kiasi kwamba injili haikuathiri matendo yao. Wengi wa watu hawa hawakuwa Wakristo wa kweli. Labda walikuwa wameanza maisha yao kama Wakristo, lakini kwa sasa wanaipuuza na kuikataa imani yao. Hapo mwanzo, mbegu ilipandwa na ikaanza kukua, lakini udongo ulikuwa hauna kina sana, na hivyo imani yao ilikufa. Nafikiri kwamba makanisa mengi hufanya makosa ya namna hii. Baadhi ya makanisa hufikiria kwamba wakati mtu anapoamini kuwa Mkristo, huamini kuwa kazi ngumu imeshafanyika. Ngoja nikuambie, kwa kuwa huyu mkristo mchanga, kazi ngumu ndo kwanza imeanza tu. Wakristo wanahitaji kufundishwa na kufuaswa. Wanahitaji kulishwa zaidi. Ninadhani kutakuwa na watu wengine, katika makanisa yenu ambao walifanya uamuzi wa kumfuata Kristo, lakini udongo wao ulikuwa hauna kina sana, na bado hawaendelei kumfuata Kristo – hata kama wanakuja kanisani! Kama Wakristo, tunahitaji kuwa na mizizi imara ambayo imezama chini ndani ya Kristo, kama tunataka kuvumilia katika kutembea kwetu katika imani.

**Katika mistari ya kumi na nane & kumi na tisa** Yesu anaongelea juu ya kundi la tatu la watu: *"bado wengine, ni kama mbegu iliyopandwa katika miiba, wamesikia neno, lakini wana wasiwasi wa maisha, udanganyifu wa mali, na tamaa kwa mambo mengine huja na kulisonga neno, na kulifanya lisiwe na matunda".* Inaonekana hapa kwamba wakati mkulima anapopanda mbegu, vichaka vya miiba huwa havionekani. Wakati ardhi imetayarishwa kwa ajili ya kupandwa, huenda vichaka vya miiba huwa vimechomwa moto, lakini mizizi ya miiba bado iko katika udongo. Na pale mbegu zinapoanza kukua, hivyo hivyo mizizi ya miiba nayo huanza kukua. Na pale miiba inapoanza kukua hushindania kupata hewa, maji, na mwanga, na kwa taratibu miiba huanza kuikaba mbegu, kabla ya kuzaa matunda. Kwa maneno mengine, mbegu hukua na kuwa mimea – lakini sio mimea yenye afya. Haiwezi kuzaa matunda yoyote.

Yesu anazungumzia juu ya miiba kuwa ni mambo matatu. Angalia katika **mstari wa kumi na tisa**: *"wasiwasi wa maisha haya, udanganyifu wa mali, na hamu ya mambo mengine"*. Wasiwasi. Mali. Tamaa. Mambo hayo huusonga mmea na kuufanya uwe dhaifu. Kwa maneno mengine, hii inaelezea juu ya mtu ambaye ana moyo uliogawanyika. Huyu ni mtu ambaye ni Mkristo, na ambaye amekuwa akijaribu kumfuata Kristo, lakini wasiwasi wa maisha haya humzuia kuwa mtu aliyetoa kikamilifu. Nafikiri jambo hili linawaelezea watu wengi katika makanisa yetu. Wao ni Wakristo - lakini namna wanavyoishi maisha yao, na maamuzi yao wanayoyafanya wala hayamwonyeshi Yesu. Mungu si kipaumbele katika maisha yao. Wamechanganywa na kuvurugwa sana na mambo ya ulimwengu huu. Hapa kuna swali la uchokozi. Je, ni muda gani tunaoutumia kuangalia TV? Je, tunatumia muda gani kwenye simu zetu kila siku? Na kisha jiulize swali hili: Je, ni muda gani huwa unautumia kusoma Biblia yako au kuomba? Ni shughuli gani iliyo na kipaumbele? Ni vitu gani katika maisha ambavyo hukuchukulia muda mwingi sana, na kukuzuia katika kumfuata Kristo zaidi? Unaona, kama **mstari wa kumi na tisa** anavyosema, "*tamaa ya mambo mengine huja na kulisonga lile neno, na kulifanya lisiwe na matunda*". Matokeo yake, Wakristo wa hivi wasongi mbele katika imani yao, hudumaa katika ukuaji wao.

Yesu pia anazungumzia juu ya udanganyifu wa utajiri. Je, mtazamo wako ni upi juu ya fedha, na jinsi gani unazitumia pesa zako? Jinsi tunavyotumia fedha zetu, kama Wakristo, ni mojawapo wa njia tunazoweza kuonyesha vipaumbele vyetu ni vipi katika maisha. Je, tumedanganywa na mali? Je, tunatamani fedha zaidi na zaidi katika maisha yetu. Wakati mwingine inahisiwa kwamba tunaishi katika jamii, ambayo imejaa uroho na uchoyo ambapo watu hutaka tu kuwa na pesa zaidi na zaidi, ili waweze kuzitumia wenyewe. Katika nchi za Magharibi, watu wengi wanataka kutumia fedha zao kwa furaha, na wanataka kutumia fedha zao wenyewe tu binafsi - na si wengine. Je, mtazamo wako dhidi ya fedha ni upi?

Tumeshalingalia somo hili huko nyuma katika semina zetu. Suala la fedha. Kupenda fedha na mali. Suala hili ni jaribu kwa viongozi wengi wa Kanisa leo. Tunasikia habari nyingi katika Kanisa kwamba fedha zimepotea, kwa sababu watu wameziiba. Katika baadhi ya makanisa, hapa Tanzania na duniani kote, baadhi ya wachungaji wamekuwa wakiwaibia watu wao. Baadhi yao wame-jikusanyia kiasi kikubwa cha fedha kwa njia ya sadaka. Wameitunza fedha wao wenyewe na kuwa matajiri sana. Baadhi yao wamefichuliwa wazi, na wamekamatwa na kupelekwa mahakamani. Baadhi yao wako hata gerezani, na matokeo yake, wengi wamepoteza na kuharibu sifa zao, huduma zao, na hata ndoa zao. Tatizo la fedha ni kwamba inaweza kuupotosha moyo, kwa kiasi kwamba unakuwa na tama ya kupata zaidi na zaidi katika maisha yako. Kwa mara ya kwanza, mwizi anaweza kuiba kiasi kidogo tu, na kama hakuna yeyote atakayemjua, hujaribu tena. Na taratibu, baada ya muda fulani, huanza kuiba kiasi kikubwa, na hatimaye hufikia hatua ya kutoweza kuacha.

Tatizo hili limekuwa kama madawa ya kulevya kwao. Wanataka zaidi na zaidi. Mtume **Paulo** anaonya kuhusu tatizo hili katika barua yake ya kwanza kwa **Timotheo**. Turejee katika Barua ya Kwanza wa Paulo kwa **Timotheo**, **sura ya sita, mistari ya tisa na kumi**, kwa sababu ninataka sisi tuone dhahiri kile kinachosema: *"watu ambao wanataka kupata utajiri huanguka katika majaribu na mtego, na katika tamaa nyingi za kijinga na zenye kudhuru, ambazo huwaweka watu katika maangamizo na uharibifu. Kwa maana kupenda fedha ni shina la kila aina ya uovu. Baadhi ya watu ambao wana hamu ya fedha, wame-jitengana na imani, na kujichoma wao wenyewe katika masikitiko mengi".* Jihadhari na majaribu ya fedha na mali, kwa sababu huisonga na kuikaba imani yako, na maisha yako.

Tafadhali usifikiri hili siyo tatizo katika Kanisa – ni tatizo kabisa. Na lazima wewe uulinde moyo wako dhidi ya hili. Huwa ninashangazwa daima ninaposoma habari za **Yuda Iskariote** katika injili. Huyu ni mtu ambaye alikuwa ametumia **miaka tatu** pamoja na Yesu na wanafunzi wengine. Alikuwa ameyasikia mafundisho ya Yesu. Walikuwa pamoja kama kikundi, wakiomba na kufanya huduma kwa pamoja. Hata walitoka nje na kuwatolea watu mapepo wakiwa katika safari za huduma! Na bado tunajifunza kwamba mwanafunzi huyu alikuwa mwizi! **Yohana** anatuambia hivyo katika injili yake. **Yohana sura ya kumi na mbili** inasema hivi: "*Yuda alikuwa mwizi. Kama mtunza mfuko wa fedha, alikuwa akiiba kile kilichokuwa kikiwekwa ndani yake".*

Unaona, inaweza kutokea katika Kanisa. Inaweza kutokea katika kundi la watu, ambao hata walitumia muda wakiwa na Yesu. Na bila shaka tunajua hata mambo mengine aliyoyafanya. Alipenda fedha sana kwa kiasi kwamba alienda kwa viongozi wa Kiyahudi na kukubaliana bei ya kumsaliti Yesu – na kwa usaliti wake, alijikusanyia vipande **thelathini** vya fedha. Kupenda fedha kunaweza kuwafanya watu wafanye mambo maovu. Kila mtu anapaswa kujua kwamba kupenda fedha kunaweza kuathiri maisha ya Kikristo. Hatimaye angalia katika **mstari wa ishirini**. *"Wengine, ni kama mbegu zilizopandwa kwenye udongo mzuri, husikia neno na*

*kulikubali - na kuzalisha mazao; mbayo ni thelathini, sitini au hata mara mia moja ya kile kilichokuwa kimepandwa".* Mstari huu unamzungumzia mtu anayeiitikia habari njema ya injili kwa furaha; huyatoa maisha yake kwa Mungu; anamfuata Yesu kwa moyo wake wote, na kisha huliruhusu Neno la Mungu liende na kuzama ndani zaidi katika maisha yao. Hii inamwelezea Mkristo ambaye anakua na kukua, na anaendelea kuzaa matunda katika maisha yao na katika huduma zao. Huyu ni Mkristo ambaye ni mtiifu kwa Mungu, na ambao hutaka kukua katika imani yao.

Na tunapoelekea kuhitimisha, hebu turejee katika kitabu cha **Luka sura ya nane, mstari wa kumi na tano**. Luka pia anatuambia kuhusu "Mfano wa Mpanzi", lakini anaongeza kitu hapa ambacho ninafikiri tunahitajika kukiona. "*Lakini mbegu katika udongo mzuri husimama kwa wale walio na moyo mwema na mnyofu, ambao hulisikia neno, na kulishika, na kisha huzaa matunda kwa kuvumilia*". Neno '**kuvumilia**' ni neno muhimu kwetu. Kuishi maisha ya Kikristo yenye kuzaa matunda na mazuri, daima si jambo rahisi – kwa kweli, kuna majaribio na majaribu; kuna ugumu na vita vya kupambana navyo. Lakini, kwa kulishika Neno la Mungu; kwa kuliruhusu Neno Lake liende ndani katika maisha yetu; kwa kuvumilia na kukaa imara, tunakua kama Wakristo. Wakati mwingine tunapaswa kwenda vitani dhidi ya miiba katika maisha yetu, lakini pale tunapovumilia, tunakua, na pale tunapokua, tunazaa matunda mengi katika maisha yetu. Nafikiri Mungu hufurahia sana wakati anapowaona watoto wake wakizaa matunda, hata wakati ambao ni mgumu kufanya hivyo.

Tunapohitimisha, tuna mambo **matatu** ya kufikiria. **Kwanza**, kama wewe uko katika aina tatu za kwanza za udongo; kama udongo ule ndiyo unaokulezea ulivyo – basi unapaswa kutubu, na kufanya kitu kuhusu jambo hilo. Kama wewe uko katika kundi la **nne**, udongo ambao ni mzuri, na kama wewe unazaa matunda – endelea kukua; endelea kuvumilia, na kuliruhusu Neno la Mungu liingie ndani katika maisha yako. **Pili,** hapa kuna swali kwa ajili yako. Je, watu wa kanisani kwako hukuangalia na kukuona akizaa matunda? Je, wanafikiri kwamba unakua na kuimarika kama Mkristo, au wanakuona kama mtu ambaye unasumbuliwa na mambo mengi? Je, wanakuona kama mtu uliye na tamaa ya kupata fedha zaidi kuliko injili? Na **tatu**, Je, unafanya kazi ya mkulima wa kiroho? Je, unapanda mbegu ya injili? Je, unawaambia wengine kuhusu habari njema ya Kristo? Kama mkulima na mchungaji, Je, unawalisha watu wako chakula bora cha kibiblia? Ninatumaini unafanya hivyo.

-----------------------------------------